**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA UYUI**

**SHULE YA SEKONDARI TURA**

FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE.

Mkoa Wa Tabora
Wilaya ya Uyui
**Shule ya sekondari Tura**

***baruapepe*** : *tura.sec3118@gmail.com*

Kata ya Tura
Barabara ya **Magufuli**
P. O . BOX 1186
UYUI
**TABORA**

***Tarehe*** 20.04.2024

SIMU 1. ***Mkuu wa Shule 0784166151/0754270733***
2. ***Makamu Mkuu wa Shule 0672527679***
3. **Mwandamizi taaluma 0656017247**
4. **Mwandamizi malezi 0765351149**

---

MZAZI/MLEZI WA ..............................................

S. L. P..........

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI TURA HALMASHAURI YA WILAYA YA UYUI MKOA WA TABORA MWAKA 2024.**

1. Ninayo furaha kukujulisha kwamba mwanao ......................................... Amechaguliwa kujiunga na kidato cha TANO (BWENI) katika shule hii kwa mwaka huu wa masomo 2024. Hivyo nachukua fursa hii kukupongeza sana wewe na mwanao.

2. Shule ipo km 149 toka Tabora mjini kuelekea ITIGI. Shule ipo Mkoa wa Tabora, Wilaya ya Uyui, Tarafa ya Igalula, Kata ya Tura. usafiri wa kufika shule unapatikana muda wote. Namna ya kufika shuleni,
   (a) Kwa watakao tokea mikoa ya Kagera, Mara, Geita, Mwanza, Kigoma, Katavi, Shinyanga, Simiyu watashukia Stendi ya mabasi Tabora. Nakupanda kosta za kwenda Tura nauli ni shilingi 7,000/=.
   (b) Kwa usafiri wa basi la moja kwa moja kutokea Dodoma, iringa, mbeya, Morogoro, Dar es salaam shuka stendi ya Tura.
   (c) kwa wale wanaotokea mikoa ya Kilimanjaro, Arusha,

Tanga, Manyara, Singida njia fupi ni kupitia manyoni hadi Stendi ya Mabasi Tura nauli kutokea Manyoni hadi Tura ni Tsh. 10,000/=

(d) Kwa wale watakao tumia usafiri wa treni washukie stesheni ya Tura na sio Tabora mjini.

3. Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **30.06.2024** kwa ajili ya usajili tayari kuanza masomo kwa muhula wa kwanza tarehe **01.07.2024** na mwisho wa kuripoti kwa mwanafunzi zingatia tamko la serikali la TAMISEMI litakalotolewa.

4. Mara upatapo barua hii na kuisoma kwa makini, tafadhali unatakiwa kumpatia mwanao mahitaji yote stahiki (yaliyo orodheshwa) ili kumwezesha afike shuleni mapema bila kupoteza muda wa masomo.

5. **SARE YA SHULE**

(i) Sketi 2 rangi ya **light blue** ndefu usawa wa kisigino. Aina ya mshono ni **rinda box (kama ilivyo kwenye picha)**.

(ii) Shati 2 rangi nyeupe mikono mirefu.

(iii) Gauni ndefu(shamba dress) ya **dark blue** mbili yenye marinda mapana.

(iv) Viatu vya ngozi jozi 2 vyeusi vyenye mkanda mmoja.

(v) Sweta rangi ya **light blue** wakati wa baridi (Jacket/Koti haviruhusiwi.

(vi) Soksi ndefu jozi 2 nyeupe.

(vii) Viatu kwa ajili ya michezo (RABA NYEUSI)

(viii) T-shirt 2 za damu ya mzee zenye kola (Fomu six)

(ix) Shuka jozi mbili rangi ya pinki.

(x) Truck suit ya kijivu kwa ajili ya michezo. (kama ilivyo kwenye picha)

(xi) Kwa Wanafunzi wa kiislam hijabu ya darasani ni **rangi nyeupe** na hijabu ya kushindia ni rangi ya **pinki,** hijabu na sketi zao sharti ziwe ndefu. (Sketi ziguse visigino).

(xii) Tai ya mistari -light blue na nyeupe

## 6. MAAGIZO MENGINE YA JUMLA KWA BWENI NA DARASANI

(a) Godoro la sponji (futi 6 x futi 2½), zinapatikana maduka ya jirani na shule

(b) Sanduku la chuma (kuhifadhia vifaa vyake)

(c) Mto mmoja wenye foronya ya pinki na blanketi

(d) Mswaki na dawa ya kutosha muhula mzima

(e) Sabuni ya kufulia na kuogea za kutosha muhula mzima.

(f) Vifaa vya kulia chakula(sahani,bakuli, kikombe na kijiko) visiwe plastic

(g) Ndoo mbili (Plastic lita 10)

(h) Fedha ya matumizi madogomadogo (**Pocket Money**), ikizidi elfu 50,000/= akatunziwe ofisi ya malezi.

(i) Jozi moja ya khanga au kitenge na taulo.

(j) Aje na madaftari Counter Book (Quire 4) ya kutosha masomo yake.

(k) Aje na Mathematical set, Kalamu pamoja na Calculator (Scientific) kwa masomo ya sayansi.

(l) Aje na vitabu vya masomo yake binafsi (Orodha ya vitabu imeambatishwa).

(m) Aje na net nyeupe kwa ajili ya kuzuia mbu.

**(n)** Nguo za nyumbani pamoja na simu (aina yoyote) **HAVIRUHUSIWI.**

(o) Nywele fupi - Hakuna kusuka wala kutia dawa.

(p) Njoo na rimu A4 mbili kwa muhula.

(q) Njoo na Result Slip, Cheti cha kuzaliwa au Affidavity Form.

(r) Aje na Dissecting kit kwa wanafunzi wa **Biolojia**.

## 7. MAAGIZO YA FEDHA NA VIFAA VYA USAFI NA MAZINGIRA

### A: MICHANGO MUHIMU

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB:** Fedha za michango muhimu kipengele "A" zote zilipwe Benki Akaunti Namba **51010061395 NMB-(TURA HOSTEL GROUP ACCOUNT**).

**B: VIFAA VYA USAFI**

i) Jembe lenye mpini

ii) Kwanja (Fyekeo)

iii) Ufagio wa chelewa wa kufagilia wenye mti mrefu

iv) Soft broom (Fagio laini wa ndani)

v) Mopper.

vi) Reki yenye mpini

vii) Squiza

## 8. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Kwa vile shule ni ya serikali, inafuata na kuzingatia sheria na kanuni zote za nchi kuhusu Elimu, kama zinavyosomeka kwenye Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia pia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.

Utakapofika shuleni utapewa nyaraka zinazoelezea na kufafanua Sheria, Utaratibu na kanuni za shule ambazo utatakiwa kuzifuata wakati wote utakapokuwa shuleni.

Pia utatakiwa kujaza fomu muhimu zitakazokuwa zimeambatishwa na Sheria hizo (moja wapo zikiwa ni zile za Uraia na ya vipimo) (Medical Examination) na kuzirudisha shuleni. (**HAKIKISHA MTOTO ANAPIMA AFYA YAKE**)

## 9. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 iliyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Tekinolojia yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais -TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu, unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

(c) Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation).

(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani au nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

(i) Kutunza mali ya umma.

(j) Ni marufuku mwanafunzi kutunza vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari

(k) mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshauri mwnanfunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni

**MUHIMU:**

- **unashauriwa kumufungulia mtoto akaunti ya NMB au CRDB banki kwa ajili ya kutunzia na kumutumia fedha zake za matumizi.**
- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mzazi/ Mlezi wa mwanafunzi unaruhusiwa kuja kumtembelea mwanao kwa siku itakayopangwa na uongozi wa shule ambayo itakuwa ni mara moja kwa mwezi mzima jumamosi ya mwisho wa mwezi. Tafadhali usije na vyakula vya aina yoyote kama vile chips, maji, juisi n.k. Muda ni kuanzia saa 2 asubuhi hadi saa 10 jioni.**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).
- **Unashauriwa kumkatia mtoto bima kubwa (NHIF) ya Tsh. 50,400/= au fika nayo shule utamfungulia shuleni**

## 10. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUKUSABABISHIA KUSIMAMISHWA AU KUFUKUZWA SHULE

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni;
vii. Kuwa na kucha ndefu pamoja na kuzipaka rangi.
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuolewa;

xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni, kumbi za starehe;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kutoka nje ya shule pasipokuwa na kibali maalumu.
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

NAKUTAKIA SAFARI NJEMA YA KUJA SHULENI TURA SEKONDARI
KARIBU SANA.




ADAM SHABAN MANGAO
MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI TURA.

**ANGALIZO: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia yamitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamishakuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA.**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA UYUI**
**SHULE YA SEKONDARI TURA**

## FOMU YA MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE

Mimi.................................. Mzaz/Mlezi wa Mwanafunzi aitwaye ............................

Nimesoma na kuzielewa sheria, Kanuni na Taratibu za shule na nimekubaliana nazo kama Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi na niko tayari kuzitekeleza sheria hizo pamoja na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.

________________________

**Mzazi / Mlezi wa Mwanafunzi**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA UYUI**
**SHULE YA SEKONDARI TURA**

**A: FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili la Mwanafunzi...........................................................
2. Tarehe ya kuzaliwa...........................................................
3. Mzazi / Mlezi...........................................................
4. Uhusiano na Mlezi...........................................................
5. Mahali mzazi/mlezi anapoishi. Mkoa..................................
   Wilaya..................... Kijiji/Mtaa........................
6. Mawasiliano ya Mzazi/Mlezi..........................................
7. Kabila..................................... Dini......................................
8. Kazi ya Mzazi/Mlezi.......................................................
9. Wazazi wako hai au wamefariki (weka alama √)

   . Baba Yupo Hai ( ) Baba Amefariki ( )
   . Mama Yupo Hai ( ) Mama Amefariki ( )

10. Ndugu wengine wa karibu na Mzazi/Mlezi ambao wanaweza kutumika Kama walezi wa mwanafunzi kama Mzazi/Mlezi husika hayupo.

(a) JINA.....................................SIMU.....................Mahali.....................
(b) JINA. ....................................SIMU.....................Mahali.....................
(c) JINA......................................SIMU....................Mahali.....................
(d) JINA.. ....................................SIMU...................Mahali........................

**NB**: Weka picha (passport) kulingana na ulivyojaza hapo juu

| (a) | (b) | ( c) | (d) |
|---|---|---|---|
| | | | |

**B: MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI**

Mimi (Jina la Mwanafunzi)...................................................

Nimesoma na kuelewa sheria, kanuni na taratibu zote za shule ya bweni, na niko tayari kuzitekeleza kwa muda wote nitakapokuwa hapa shuleni kama mwanafunzi. Nitakapokiuka kipengele chochote cha shule hiyo adhabu stahiki ichukuliwe dhidi yangu kwa mujibu wa sheria na taratibu.

................................. ............................

**Saini ya Mwanafunzi** **Mkuu wa Shule**

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**UYUI DISTRICT COUNCIL.**
**TURA SECONDARY SCHOOL**

P.O. BOX 1186,
**TABORA**

**Date: ...............**

## FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

**This form must be completed by a Government Medical Officer**

Student's full name.................................................

Present Age.................................................

Blood Test...........................................

Stool Examination.......................................

T.B. Test.....................................................

Asthma.....................................................

Eye Disorder.....................................................

Nose Disorder.........................................................

Ear Disorder.................................................

Skin Disorder..................................................

Anemia...........................................................

Chest..........................................................

Operation.........................................................

Serious Accidents........................................................

Any other infections disease..............................................

Pregnancy......................................................................

**Additional information e.g. Physical defects or impairment, chronic or family disease etc.**

**.....................................................................................................................**
**.........................................................................................**

**I certify that I have personally examined Mr./Miss.................................**
**And found her fit or unfit to pursue studies.**

**Signature.................................** **(Official Stamp) ....................**

**Designation.....................................**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI TURA**

## MAAGIZO MUHIMU YA VITABU VYA KIADA NA ZIADA

Ili Mwanao aweze kupata ELIMU BORA na kufikia kiwango kinachotakiwa na shule anapaswa kuwa na vitabu. Ifuatayo ni orodha ya baadhi tu ya vitabu ambavyo anapaswa kuja navyo ili aweze kumudu sawa sawa mchepuo wake.

ORODHA YA VITABU vifuatavyo hutumika kufundishia na kujifunzia katika shule za sekondari kwa kidato cha tano na sita. Kila mwanafunzi anatakiwa kununua baadhi ya vitabu hivyo kwa kila somo kwa masomo aliyopangiwa yaani PCB (Physics, Chemistry na Biology),GS (General Studies), PCM(Physics,Chemistry na Advanced Mathematics ) na EGM(Economics,Geography na Advanced Mathematics) kwa wote. (HAKIKISHA UNANUNUA WALAU KITABU KIMOJA KWA KILA SOMO)

**1. PHYSICS**

1. Principles of Physics by S. Chand Class XI & XII
2. Principle of Physics by M. Nelkon
3. Physics Form 5 & 6 by TIE

**2. BASIC APPLIED MATHEMATICS**

1. Basic Applied Mathematics (5&6) by T.I.E

**2. ADVANCED MATHEMATICS**

1. Advanced Mathematics (5&6) by T.I.E
2. Advanced Mathematics Chand's 1 & 2
3. Advanced Mathematics book 1 & 2 By Backhouse

**3. CHEMISTRY**

1. General chemistry (T.I.E)
2. Physical Chemistry (T.I.E)
3. Organic Chemistry - A. Abdullah et. Al. A Level and 1st yearUndergraduate students Vol. III Part A.
4. Organic Chemistry - A. Abdullah et. Al. A Level and 1st yearUndergraduate students Vol. III Part B.
5. Inorganic Chemistry Part A - J. S. Maro
6. Inorganic Chemistry Part B - J. S. Maro

**4. GENERAL STUDIES**

1. General Studies for Advanced Level Certificate, Form 5 - Richard R. F. Mbalase
2. General Studies, Supplementary Book for Advanced Level and Colleges, 2nd Edition - Konrad Adenaker Stiftung.
3. Bigirwamungu, J & Deogratius S. M (2012) Understanding Advanced

Level General Studies; Advanced Level Secondary Schools.

4. Nyangwine, C. M, Bukagile, G. R & Maluka, S. O (2010) Contemporary Approach for Advanced Level; General Studies Notes for 5 & 6

**5. GEOGRAPHY**

1. A Comprehensive Approach to PHYSICAL GEOGRAPHY for Secondary School by D. T. Msabila
2. An integrated Regional studies on human & economic geography. Advanced level paper 2, D.T MSABILA.
3. Monkhouse, F (1975), Principle of Physical Geography, Education Hodder
5. Regional Geography - Nyambari Nyangwine
4. Photography Interpretation and Elementary Surveying for Secondary Level New Edition - Dura
6. Certificate Human and Economic Geography - Morgan and Leong chang

**6. BIOLOGY**

1. Biology for Advanced Level secondary schools form 5 (T.I.E)
2. Biology for Advanced Level secondary schools form 6 (T.I.E)
3. Biological Science; Cambridge University Press (1997) 3rd Edition

**4. ECONOMICS**

1. Micro-economics for Advanced secondary schools, T.I.E (2022)
2. Essential for A – level Economics paper I , ABROS ODHIAMBO

## VIELELEZO VYA SARE ZA SHULE

a. (i) Sare za darasani (kawaida-**SKETI SHONA RINDA BOKSI**)





(ii) sare za darasani( t-shirt- **SKETI SHONA RINDA BOKSI**).



b. Mavazi ya jioni



C. Michezo

